

Makamu wa Rais, Dk Philip Mpango akizungumza na jumuiya ya Watanzania wanaoishi nchini Hungary, jijini Budapest jana. (Picha na Ofisi ya Makamu wa Rais).

HABARI LEO UK2.

Samia kukabidhi boti 160, kuzindua bandari ya uvuvi

Na Kennedy Kisula, Kilwa

R AIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kukabidhi boti 160 za uvuvi na kuweka jiwe la msingi kwenye ujenzi wa bandari ya uvuvi atakapofika wilayani Kilwa mkoani Lindi.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alisema hayo juzi wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufanya ukaguzi wa mradii wa ujenzi katika eneo la

bandari iliyopo Mji wa Kilwa Masoko wilayani hapa.

Alisema boti hizo 160 zenyet thamani ya Sh bilioni 11.8 ni kwa ajili ya wavuvi wadogo wadogo na wakulima wa mwani amba ni wanawake kwenye mikoa ya Pwani, Lindi, Mtwara na Tanga.

Kwa mujibu wa Ulega, wavuvi wadogo wadogo na wakulima wa zao la mwani watakabidhiwa boti 34 na Rais atakapofanya ziara wilayani Kilwa mkoani Lindi na kuwa ukanda wa Pwani

utapata boti 90 na zilizosalia 70 zitasambazwa kwa wavyuvi wadogowadogo Kanda ya Ziwa Nyasa, Tanganyika na Victoria.

Ulega alisema kwa upande wa mradi wa ujenzi wa bandari ya uvuvi ataweka jiwe la msingi na kuwa mpaka sasa ujenzi wake ulishafikia asilimia 22 na kuongeza kuwa mradi huo wa bandari utakuwa mkombozi na kichocheo cha uchumi wilayani hapa.

Aliongeza kuwa meli kubwa za uvuvi zilizokwuwa

zikivua samaki bahari kuu zilikuwa zinakwenda visiwa vyaa SheliSheli kuchakata sasa zitafanyika Kilwa.

Ulega alisema baada ya kukamilika ujenzi wa bandari ya uvuvi, sekta hiyo itachangia asilimia 10 ifikapo 2036 kutoka asilimia 1.8.

Kwa mujibu wa Mfawidhi wa Mali ya Kale wilayani Kilwa, Mess Mbogwa, ujenzi wa bandari hiyo utakapokamilika utafungua mlango na kuongeza watalii hasa kwenye magofu ya kale yaliyopo Kilwa Kisiwani.